

# Kanisa la Kristo Sio Dhehebu

(Sehemu ya Pili)

Kanisa la Kristo ndilo lile la karne ya kwanza. Na tunaweza kuthibitisha hayo kupitia sifa za Kanisa la Awali na sifa tulizo nazo.

Kanisa La Karne Ya Kwanza	Kanisa La Karne Ya Ishirini Na Moja
a) Majina ya Kanisa: Kanisa la Kristo - Rum. 16:16 Kanisa la Mungu - 1 Kor. 1:2 Kanisa la Bwana - Mdo. 20:28.	a) Kanisa la Kristo la leo linatumia jina lile linalopatikana katika kitabu cha Warumi 16:16. Kwa hiyo tunatumia jina lile Wakristo wa karne ya kwanza walikuwa wakitumia jina hilo.
b) Madaraka: Maaskofu, Washemasi, Wahubiri na Washiriki walikuwepo kwenye makusanyiko kama watu walikuwa na sifa za kazi, Fil. 1:1.	b) Leo taratibu ya viongozi kwenye Kanisa ni lile lile, hakuna mabadiriko.
c) Ibada: Walikutana siku ya kwanza ya juma, 1 Kor. 16:2. Waliimba sifa kwa kutumia midomo tu, Efe. 5:19. Waliomba, walihubiri, walichukua meza ya Bwana na walitoa changizo, Mdo. 2:42, 47; 1 Kor. 14:15; 16:2; Mdo. 20:7.	c) Kanisa la Kristo leo linakutana kila siku ya kwanza ya juma. Katika ibada tunaiimba bila vyombo vyao muziki, tunaomba, tunashiriki Meza ya Bwana na tuna toa kama karne ya kwanza.
d) Mwongozo: Walifuata mafundisho ya mitume kwa mamlaka ya imani na matendo yao, Mdo. 2:42; Gal. 1:6-9; Ufu. 22:19.	d) Kanisa la Kristo leo linaongozwa na mafundisho ya mitume tu, hatuna mwongozo zaidi ya Agano Jipy.
e) Kama Ultaka Kujunga Nao: Ni lazima uamini, utubu, umkiri Kristo na kubatizwa na maji mengi, Mdo. 8:26-40.	e) Vile vile leo hatuna tofauti hata kidogo, tuko sawa kabisa.
f) Huduma: Kushika yaliyo kweli katika nyumba ya Mungu, 1 Tim. 3:15.	f) Kanisa la Kristo leo linashika maneno ya Yesu na Mungu kama ilivyo kweli yote, hatuongezi au hatupunguzi hata kidogo.

## Hitimisho:

Kitu kinachofanyika kwa ujumla, siyo kwa sehemu tu. Kwa hiyo unaweza kuona Kanisa la Kristo la leo si kwamba linafanana au likokaribu na Kanisa la Awali, bali Kanisa la Kristo la leo ni Kanisa la Awali, hakuna tofauti hata kidogo. Kwa hiyo kwa sababu tuko sawa basi sisi pia ni Kanisa la Kristo.